Tuzungumze

# Wachungaji na siasa katika makanisa

Siasa na injili ni mambo mawili yaliyo tofauti katika matumikio yake. Ila tuseme ya kuwa siasa ya kweli yatoka kwa Mungu sababu hiyo ni njia moja wapo ya kuweza kuongoza watu katika taratibu na hekima ya Mungu. Ikiwa siasa ya nchi ZAIRE kaenda mbali na mapenzi ya Mungu baada ya muda mrefu, vivyo hivyo makanisa mengi yaanza kutoka katika msimamo unao ruhusiwa na Mungu. Na labda ulio msinji wa mambo hayo ni wachungaji na huduma pia tabia zao kwa kundi. Wengi badala ya kuchunga kanisa walitawala na hivyo wajitia kwa nafasi ya Yesu aliye kichwa cha kanisa. Pahali pa kufanya huduma wao, wamoja watawala, wachunga na waongoza. Lengo na shabaa yao vyaelekea sasa kwa vitu na kutia tumaini lao katika maendeleo na kujijengea manyumba pahali pa kuendelesha watu kiroho. Na hivyo siasa yaingia sana katika makanisa.

Tatizo ni kuona hata watumishi wajifanya kuwa sasa wanasiasa, si kwamba wanavyo vitambulisho vya chama ao (cartes de membre) bali nia na tabia pamoja na matumikio yao yaonyesha sasa kama siasa (...) tayari yatawala makanisani. Ebu, jaribu kupinga na tukuonyeshe yalivyo. Katika mji wa Bukavu na nchini Zaïre kuna wachungaji walio wanamemba wa vyama vya siasa. Wamoja ni wanamemba wa PDSC, wengine wa UDPS, na wengine wakiwa wa "Société civile" ambako wana madaraka makubwa sana. Majina yao yajulikana labda na wengi.

Tulipo hojiana na mchungaji Lukeba aliye prezidenti wa ECZ kuhusu mambo hayo, huyo katoa maoni na mashauri yake ili kuwasaidia watumishi na wakristo wote kuhusu siasa. Bwaba Lukeba Mulamba kaleta umbalimbali ulioko katika mkristu na mwanasiasa. Kwa kifupi, mkristu ni yule ashikae neno la Mungu kupita Yesu Kristo akimtumikia na kutegemea ujio wake na kuacha zambi. Mwanasiasa ni yule agombeaye madaraka ya nchi na kuishughulikia kwa shabaa ya kutawala. Bali mkristu kama vile "laïc" aweza katetea nchi yake kwa njia ya kumtii Mungu. Isiyowezekana ni kuona mtumishi yeyote ao mchungaji kuwa mwanasiasa wala kupendelea chama fulani sababu aweza kugawa kundi alilo nalo. Kweli mpastori ajiingizae katika siasa sherti ajirekebishe ao aamue katika msimamo wake. Ni kwa neno la Bwana Yesu kanena "hakuna mtu awezaye kuwatumikia mabwana wawili..."Ebu sasa hakuna watu wamtumikiao Mungu na mali ? Ikiwa ni hivyo mambo hayata-changanywa ? Mchafuko hamuna makanisani ? Katika makanisa hamuna vikundi viitwavyo pia "mouvance présidentielle" na "acquis au changement?" Hakuna ukabila na matengano kanisani ? Twaenda wapi? Ndio sababu mambo ya kimwili na sheria vyatawala kanisani ila Yesu alikuja kuweka kanisa huru. Mawazo ya wanadamu ndio yatawala kuliko uongozi wa Roho Mtakatifu. Angalisho, sababu hukumu itaanzia nyumbani mwa Mungu.

Katika kuhubiri kwake mwinjilisti Julias Heri kanena "wakati umefika ambao mtu yeyote ikiwa hata simama katika Yesu Kristo atapata shida na taabu kubwa kimwili pia kiroho. Lazima aliye na imani aishi kwa imani na matendo kwa ajili ya Mungu, na ikiwa ataishi sherti mwenye zambi afe kusudi hakutii neno la Mungu. Huu ndio wakati wa mavuno na kubagua kondoo na mbuzi. Ezekieli 18 : 20". Sasa mkristu mwenzangu, mchungaji rafiki, ikiwa Yesu katambua hayo na kuona hofu katika siku za mwisho mambo yatakavyokuwa, anauliza : "Atakaporudi mwana wa Adamu, je ! ataiona imani duniani ? Fikiri wapi uliko sasa.

**Mutungwa A. Phóly**

Neno la wasomaji

# Wachuuzi wa Salamabila watetemeshwa

Jua mpenzi,

Ni mara ya kwanza nachukuwa kalamu yangu kwa kukuandikia kutokana na vitisho vyatushambulia toka viongozi wa hapa Salamabila. Na ninatumaini kama utaweza kunitolea mawazo kwa jambo hilo. Kwa kweli sisi wachuuzi "ambulants" wa kabila ya Bashi tuasumbuliwa sana hapa Salamabila na vitendo vya wa "commissaires de zone".

Kila siku iyendao kwa Mungu, tunaombwa kulipa kodi (taxes) mbalimbali tusijuwe msinji. Mfano wangu siwa pekee bali pia wa wengine ndugu wachuuzi. Kwangu mwenyewe nimekwisha toa feza kwa kulipa "taxes" 40 tangu mwezi wa inne. Kwa siku ya leo ndio ya maajabu. Kila muchuuzi Mushi anapashwa kulipa 3 g ya zahabu (d'or) ao zaïre 180.000.000.

Eti pesa hizo ao zahabu twatoa itatolewa kwa Raïs Mobutu kama vile zawadi wakati atafika kutembelea jimbo la Maniema akifikia mjini Kindu. Taxe hiyo yaitwa "accueil présidentiel". Ulizo langu ni hili : kama Raïs Mobutu atembelea jimbo ao mji fulani, wakaaji wapashwa kukongoa feza ama vinginevyo vifaa ama ile mwaita katika kifransa "collecte" ya kumpatia ?

Sisi wachuuzi wa "ambulants" tunasagwa gongo na makonde na kutupwa gerezani sawa wanyama juu ya jambo hilo. Basi, kama munajibu kwa ulizo mukanitulize.

**Tchabene Mumume,**
**Commerçant pa Salamabila**

***NLMW:*** *Ndugu Tchabene Mulume, tumesikia malalamiko yenu. Nazani viongozi wa serkali jimboni na hao wa mahali mwakaa ni wasomaji wetu watukufu. Hakuna hata siku moja Raïs wa Jamhuri, Mareshali Mobutu aliweza kuwatuma viongozi kumkongolea feza na zahabu. Serkali ni tajiri. Ila tu wayanguwangu, wizi na wakorofi ndio wataka kuwinia miongoni mwa wakaaji wakitaja jina la Raïs Mobutu. Hao ni wizi tu. Na twatumaini wakuu na viongozi serkalini watasikia malalamiko yenu na watatoa jawabu. Basi, musichoke kutoa nje vitendo vya hofu vyawatukia huko. Jua, Gazeti lenu litaangaza tu.*

Kwako bibi

# Kugonda siyo kugonjwa ukimwi

Wabinti kama vile wamama, twawaomba mchagueni katikati ya kifo na mavazi kama vile Dubayi na Super-wax ! Sababu, siku hizi watu wengi wafikiri pengine mtu yeyote anayegonda sherti atajike ugonjwa wa Ukimwi (kwa kifupi upungufu wa kingo mwilini) ama Sida.

Lakini tukichungua vizuri, alama za ugonjwa wa Ukimwi ni nyingi sana : kuhara, uzaifu wa mwili, upungufu wa uzito, kuchakala, kuongoka kwa nywele, kupotelewa akili hata kufanana mwenda-wazimu, kugonjwa kifua kikuu (tuberculose) na kutapika damu, kikohozi na vivi hivi. Nchi jirani kama Rwanda, Burundi, Uganda na Tanzania zajulikana kuwa shamba za magonjwa hizo katika Bara la Afrika na ulimwenguni. Wamama wachuuzi toka Zaïre hasa jimboni mwa Kivu ya Kusini, Shaba na Kivu ya Kaskazini wajulikana kama wamojawao wa watu wanaotembeza haraka ugonjwa huo haramu kwa tabia zao mbaya za usharati na pupa ya pesa.

Siyo tu wamama bali pia wanafunzi, watalii, wabinti, wababa wasafiri na watu wengine kazaa. Si vema kuwaza kuwa ni mume ao mke mwenyi kugonda tu ndiwo waweza kuwa na ugonjwa huo. Wagonjwa wengi wa ukimwi (Sida) wanabaki na vijidudu (VIH) ama viini vya ugonjwa huo mda wa miaka mingi ijapokuwa mwili wao wabaki na hali ya kunona na kutamanisha.

Ni vema kweli tujiepushe sababu twajihatarisha sisi wenyewe na kusahau kama ukimwi bado haujapata dawa. Yajulikana kama ugonjwa wa ukimwi watawala watu wanoishi na kutembelea mji mkuu wa Kigali ambako wamama wane (4) ju ya kumi wamekwisha kuambukiwa. Pia mji wa Bujumbura, Kigoma na Dar-es-Salama, Kampala na Nairobi. Upande wa Zaïre, hasa Uvira (Mulongwe), Bukavu (nguba, Nyamugo, Essence, Pajeco na Bagira) mbegu mbaya ya ukimwi yaletwa na kupandwa hasa na wamama wachuuzi waendao nchi jirani na ambao mwendo wao ni kama ule wa wamama wakahaba (malaya). Katika kazi hiyo ya kuharibu taifa letu na magonjwa haya mabaya wamama hao, wenyi kuolewa kama vile wamalaya, wasaidiwa na wabinti waitwao kwa jina la "Kayabunde".

Lakini ni vizuri tukamilishe kama siyo wamama wote wanaotembea ovyoovyo bali wengi kati yao. Haya sana, jameni ! Basi, je, mama, itakufalia nini kupoteza roho na maisha yako hata kama unaweza "kuvuma" mda mfupi, kujengea mme nyumba, kuvaa kila mtindo wa "Dubay", kanga na Cotebu, Super-wax... ya kila rangi ? Tengeneza maisha yako, ungali na wakati ndugu. Kilio na kusaga meno ni kinyume ya kukataa mashauri.

**Imata Raphaël Déwen**

## JE, UMESIKIA ...

***Kuwa,***
mchuuzi moja wa mafuta ya taa hapa mjini Bukavu haregei na kitendo chake cha kujenga bomba la kushota "Essence" kunako "place Mulamba" ? Nia yake iliyopigwa marufuko mwaka jana na wanafunzi wa chuo cha Alfajiri na Cirezi hapo walipoandamana barabarani. Bwana huyo apendelea sasa kuuza eneo la mahali pajulikanao kwa namba SU 3969 kwa feza za dolari za kimarekani kwenye chumba cha mtaa wa Ibanda ambako mahali hapo padaiwa na diosezi ya kianglikani kuwa eneo lake kusudi ijenge masomo mahali ya sekondari ya Elimu. hata hivyo mashitaka hayo yamekwisha wafikia wakuu wa serkali na wachumba kihusikacho na mambo ya arzi. Ni bora kujua mwisho.

***Kama,***
kiongozi jimboni mwa Kivu ya kusini kawapa angalisho wafanyakazi wake wa kiserkali kuhusu sheria inayoelekea matumizi bora ya mali ya serkali. Mwito wake huo katolewa baazi ya viongozi makamu wa mitaa wa Minova na Mubone kufika hapa mjini Bukavu kueleza wazi ulaji ovyo wa mali ya serkali na viongozi wao wa mitaa ya Kalehe na Walungu. Ikiwa mambo yabadilika kulingana na nyakati, ingelikuwa vema hotuba na husuda kuacha kwa sheria na haki kutawala katika nchi.

***Kwamba,***
wakaaji wa mtaa wa Shabunda si leo watakapo furahia matunda ya demokrasia nchini Zaäre ? Popote ndani ya eneo la mtaa huo kwapatikana maboma (barriäres) za askari jeshi ambao wasumbua watu na kuwapokonya wanafunzi, wachuuzi na wasafiri wengine mali zao. Yaliyo vigumu kupita ni boma za Kitumba, Cabene, Kitindi, Kalole na Mukoloka ambako askari jeshi wakiongozwa na ma adjudants" Zidisha Kemo, Okamba na Bukuru aitwae "Farao" na atetemeshae huko. Yasemekana pia kuwa mkuu wa eneo la Wakabango I bwana Museme Nsoko Moligi hahusiki zaidi na usalama wa watu ila tu na pesa. Eh tuseme je !

***Eti,***
walichokusudia kakitenda ? Vijana wanafunzi hao wa chuo cha UEA kamshika hapo majuzi mwanahabari rafiki aliye kuwa akifurahi kutoka kwa gazeti lake. Shabaa yao ni kuona mwanahabari huyo kachafua mkuu wa chuo chao. Yasemekana pia mjini Goma kama mwanahabari mwengine angetoa maisha yake kufuatana na kitendo ambacho mkuu ahusikae na utayarishaji wa mambo kamtendea huko akimrusha ndani ya gari lake hapo waziri wa utangazaji wa habari alipo fanya ziara mjini Goma. Shujaa huyo ajifanya kuwa adui wa wanahabari. Ijapokuwa ndugu huyo alikuwa akingojelea mshahara wake wa miezi ine toka kwa waziri wake.Bwana Shoyo hakupenda kumuelewa mwenziwe. Na hayo yote yasemekana kuwa ni jambo la kusaisha wanahabari wanaojifura- hisha kazi yao. Hum !

***Kuwa,***
mwenye kiti wa muji wa Kindu ni mtu wa kipekee katika kazi ? Bila shaka bwana huyo kaamua kuchunguza vyumba vyake vya kazi mjini Kindu. Ajabu ni kuona bwana Fereza ambaye hatafanya lolote ahusika na kila jambo. Fereza achunguza hata viwanja vyakaliwa na watumishi wake. Kwake yeye, vyoo na misalani havivutii sababu ya harufu bali kwa ajili ya uchafu ambao wafaa kukomesha. Yeye binafsi kaonyesha mfano na yasemekana kuwa amri hiyo ni shurti kubwa kwa yeyote. Asiye itii huenda kalipa feza kiasi cha milioni 25 hadi 50. Ni njia ingineyo ya kuchunga usafi kwa mji.

***Kwamba,***
yapata watumishi 11 wa shirika la Sominki wamo kifungoni huko Kalima kwa kukosa adabu ? Hao kajiruhusu na kuwanasa wakuu kazaa wa shirika hilo kwa kiwango cha pesa kazaa kakawia na kuwafika ? Kando ya hiyo walipendelea kupongezwa na shirika lao. Lakini, wakati ukaidi wawashika wale wahusikao na usalama, twaweza kujiuliza kama gereza hazifai na kuchunga usalama wa mambo. Nani basi atakayewalinda walinzi ?

***Eti,***
mnamo tarehe 4 mwezi jana, yapata Kasuku 40 ya watu mbalimbali katekwa nyara wakati watu hao kajiandaa na kuzipeleka mjini Bukavu ? Kwa mshangao mkuu, sehemu moja ya ndege hao kapelekwa barani Ulaya ambao wanasheria wa Kindu kazigawa. Mjini Bukavu mateka wengine wa ndege hao kapitika kunako "Place Major Vangu" wakati zilipotayarishwa kupelekwa mjini Bujumbura. Inabidi mambo hayo ichunguzwe. Na katika ukumbi huo wa kutekwa ovyo, hakuna kundi la kimagendo ambalo lastahili kuhukumiwa vikali sana.

***Kama,***
ni mazishi ya kipekee kafanyika mjini Kindu kwa ayati Kahuma, mtumishi wa shirika la SFE ? Wafanyakazi wa shirika hilo kakusudia mnamo tarehe 7/5/1993 kuzingira mwili wa marehemu katika sanda inayofaa wakiwa mbele ya ofisi ya mkuuwa wafanyakazi wao na kudai mazishi yaliyo halali. Hata hivyo hakuna lolote lililofanyika. Ayati Kahuma kazikwa kama vile mfungwa asiye na heshima ijapokuwa barani Afrika, kuheshimu wafu ni kitendo kisichoadibishwa kwa yeyote ule. Alah !